

## ALOGUNDUA MPUNGA

1. Mchele ni punje ndogo, itokayo mpungani  
Mpunga sio kidogo, ulimwao mabondeni  
Walimao ni Wadigo, na Wazaramo wa pwani  
Alogundua mpunga , Mungu amweke peponi.
2. Mchele bila ya zogo, sifaze zimebaini  
Pika bila ya viungo, bado hunoga kinywani  
Atayebisha ni mwongo, hajui aseme nini  
Alogundua mpunga, Mungu amweke peponi.
3. Na utiwapo viungo, unapata biriani  
Mlaji hana mivungo, hata ale hadharani  
Aweza vuka ukingo, vitengwapo majamvini  
Alogundua mpunga , Mungu amweke peponi.
4. Hata kwa nyama ya mbogo, anayewindwa mwituni  
Iwe ngumu kama gogo, kwa kuanikwa juani  
Kwa wali hua kipigo, hubarizi mdomoni  
Alogundua mpunga, Mungu amweke peponi.
5. Na hata wenye mapengo, wanauona laini  
Humung'unya kwa maringo, inapotengwa sahani  
Bila mishipa ya shingo, kutoka ikabaini  
Alogundua mpunga, Mungu amweke peponi.
6. Wali kwa wake mnogo, ladhaye hutabayani  
matonge kama komango, husukumizwa kinywani  
wali jama si mzigo, hata ujae tumboni  
Alogundua mpunga, Mungu amweke peponi.
7. Burundi na hata Congo, mchele wanathamini  
Tumbatu na songosongo, wanaufata sokoni  
Huisahau mihogo, inayolimwa tutani  
Alogundua mpunga, Mungu amweke peponi.
8. bokoboko ni msongo, upendwao Arabuni  
Ni wali hupondwa gongo, uwapo sufuriani  
Wakubwa pia wadogo, hula kwa yao makini  
Alogundua mpunga, Mungu amweke peponi.
9. Hata wachezaji bingo, mashababu wa mijini  
Hubaini lao lengo, mchele kuusheheni  
Huacha yote mikogo, wakaufata dukani  
Alogundua mpunga, Mungu amweke peponi.
10. Ni radhi kutoa hongo, mchele uje nyumbani  
Au niseme uwongo, nidanganye baniani  
Ilimradi upwago, ni jiwekee ghalani  
Alogundua mpunga, Mungu amweke peponi.
11. Beti hizi si kidogo, ukweli kuubaini  
Nisitie yogoyogo, maporojo mkadhani  
Mimi siupi kisogo, mchele nauthamini  
Alogundua mpunga, Mungu amweke peponi.  
(aamin)

*Said bin Sultan*

*Box 256 pc 119*

*Oman.*

[Said\\_almughairy@hotmail.com](mailto:Said_almughairy@hotmail.com)